



Halifax

Regional Centre for Education

At-Home Reading Program

Children need plenty of opportunities to read and be exposed to books in both English and your home language. Spending time reading with your child, both you reading to your child or your child reading to you, is important to your child's reading progress. This Take-Home Reading Program will help you provide those opportunities for your child and help them grow as a reader.

Throughout the week, your child will bring home a book(s) to read. It should not take too long for your child to read the book to you, and they could even read it multiple times. They will gain confidence each time they read their book(s). Talk to your child about the book in your home language.

There may be a reading journal that your child brings home with their book(s). The reading journal provides space for you to write the date, title of the book, and comments. You can comment on if the book is too easy or too difficult or if your child enjoyed the book. This information you share in the comment section is very valuable. At the end of the week, the book(s) and journal will be collected and the teacher will read through your comments. These comments will help determine the book(s) for the upcoming week. You know your child best, so your insight is very important to the teacher.

Please know that the most important outcome of this Take-Home Reading Program is for your child to love reading. If your child is struggling, frustrated, or even just too tired to read the book one night, it is okay to take a night off. Instead, you could read the book to your child or choose a different book to read to them. Reading to your child is just as important as them reading to you. There is nothing better than enjoying a story together, especially in your home language!

Programu ya Kusoma Nyumbani

Watoto wanahitaji fursa nyingi za kusoma na kuonyeshwa vitabu vya lugha zote za Kiingereza na lugha yako ya nyumbani. Kutumia muda kusoma na mtoto wako, wewe unamsomea mtoto wako au mtoto wako akikusomea, ni muhimu kwa maendeleo ya kusoma ya mtoto wako. Mpango huu wa kuchukua na kusoma nyumbani utasaidia kutoa fursa hizo kwa mtoto wako na kumsaidia kukua kama msomaji.

Katika wiki yote, mtoto wako ataleta nyumbani kitabu(vitabu) cha kusoma. Haipaswi kuchukua muda mrefu sana kwa mtoto wako kukusomea kitabu, na wanaweza hata kukisoma mara nyingi. Watapata ujasiri kila wakati wanaposoma kitabu(vitabu) chao. Zungumza na mtoto wako kuhusu kitabu katika lugha yako ya nyumbani.

Kunaweza kuwa na jarida ambalo mtoto wako anaweza kuja nalo nyumbani pamoja na kitabu(vitabu) chake. Jarida kuhusu kusoma hutoa nafasi kwako kuandika tarehe, jina la kitabu na maoni. Unaweza kutoa maoni ikiwa kitabu ni rahisi sana au kigumu sana au ikiwa mtoto wako alikifurahia kitabu hicho. Taarifa unazo zishirikisha kwenye sehemu ya maoni zina thamani sana. Mwishoni mwa wiki, kitabu/vitabu na jarida vitakusanywa na mwalimu atasoma maoni yako. Maoni hayo yatasaidia kubainisha vitabu vya wiki inayofuata. Unamjua mtoto wako vizuri zaidi, kwa hivyo ujuzi wako ni muhimu sana kwa mwalimu.

Tafadhali fahamu kuwa matokeo muhimu zaidi ya Mpango huu wa Kuchukua na Kusoma Nyumbani ni ili mtoto wako apende kusoma. Ikiwa mtoto wako anahangaika, amechanganyikiwa, au hata amechoka sana kusoma kitabu usiku mmoja, ni sawa kuchukua mapumziko ya kusoma kwa usiku huo. Badala yake unaweza kumsomea mtoto wako kitabu hicho au kuchagua kitabu tofauti cha kumsomea. Kumsomea mtoto wako ni muhimu kama vile anavyokusomea. Hakuna kitu bora zaidi kuliko kufurahia hadithi pamoja, hasa katika lugha yako ya nyumbani!

